

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dar es Salaam
31 Agosti, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kuwa Taasisi za kidini zina wajibu mkubwa katika kulinda misingi ya familia na kujenga Taifa lenye maadili.

Rais Dkt. Samia amesema hayo leo katika hafla ya kutoa tuzo kwa washindi wa Mashindano ya Kimataifa ya kusoma Quran Tukufu kwa wasichana, yaliyoandalialiwa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kwa kushirikiana Taasisi ya World Muslim League ya Saudi Arabia, yaliyofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Aidha, Rais Dkt. Samia ametoa wito kwa BAKWATA kuweka mikakati ya kufundisha elimu ya dini kwa watoto wote bila ubaguzi na kusisitiza umuhimu wa elimu ya dini kwa wanawake kwa kuwa wanawake wana nafasi kubwa katika ulezi wa familia bora.

Vile vile, Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa, kumlea mtoto wa kike katika misingi mizuri ya kiimani kunamuandaa kuishi katika misingi hiyo. Hivyo, ni muhimu kuendelea kuimarisha familia ambayo ni misingi wa Taifa letu, ikiwemo kupitia elimu ya dini.

Akizungumzia mashindano hayo yaliyofanyika kwa mara ya kwanza hapa nchini, Rais Dkt. Samia amebainisha kuwa, kuchanguliwa kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa kwanza wa mashindano hayo ni kutokana sifa kubwa ya Tanzania ya kuishi kwa amani na masikilizano.

Rais Dkt. Samia amewataka Watanzania waendelee kulinda heshima hiyo kwa kudumisha amani na mshikamano.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Sharifa B. Nyanga".

Sharifa B. Nyanga
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu